Maswali

1. Esau alienda kuishi wapi?
2. Mungu alimwambia Yakobo aende wapi?
3. Mbona Yakobo aliogopa?
4. Yakobo alimpelekea Esau nini?
5. Nani alishindana na Yakobo kwa kivuko cha Yaboki?
6. Kulipopambazuka malaika alifanyaje Yakobo?
7. Jina mpya lenye Mungu alimpa Yakobo lilikuwa nani?
8. Yakobo alijifunza somo gani alipoanza kuchechema?
9. Nini ilifanyika wakati Yakobo alikutana na Esau?
10. Yakobo alishukuru Mungu kwa nini

Majibu

1. Esau alienda kuishi Edomu
2. Mungu alimwambia Yakobo arudi kuishi kwa nchi ya Kanaani
3. Yakobo aliogopa kwamba Esau alikuwa bado na hasira na atamua
4. Yakobo alimtumia Esau zawadi nyingi
5. Yakobo alishindana na malaika kwenye Kivuko cha Yaboki
6. Malaika aligusa paja la Yakobo na ikateguka kwa kiungo
7. Mungu alimpa Yakobo jina mpya –Israeli
8. Yakobo alijifunza kuamini kwa nguvu za Mungu – si zake mwenyewe.
9. Esau alifurahi kumwona Yakobo na wakawa marafiki tena
10. Yakobo alishukuru Mungu kwa kumrudisha salama katika nchi ya Kanaani yenye Mungu alikuwa ameahidi Ibrahimu na familia yake.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1

10 Yakobo anashindana na malaika

Kwa Biblia Mwanzo milango ya 32 na 33

Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu alimlinda Yakobo mpaka akamrudisha kwa nchi ya Kanaani. Yakobo aliweka amani na nduguye Esau.

Somo

Baada ya Yakobo kuenda Harani, Esau alikaa na Isaka na Rebeka kwa mda mfupi. Esau hakumpenda Mungu. Habari za ahadi za Mungu hazikumjalisha. Esau alioa wanawake wenye hawakumpenda Mungu. Alikuwa tajiri wa n'gombe. Alijitakia shamba kubwa. Alitengeneza jeshi ndogo alilotumia kupiga na kushinda sehemu ya Edomu, iliyo kusini ya Israeli. Esau na familia yake walienda kuishi nchi ya Edomu.

Yakobo alifanyia Labani kazi kwa miaka kumi na minne ili apate wakeze wawili – Lea na Raheli. Tena akafanya kwa miaka sita ili apate kondoo na mbuzi. Labani alimhadaa mara nyingi kwa kugeuza geuza mshahara wake. Lakini Labani aliendelea kuwa tajiri wa n'gombe, kondoo na mbuzi kwa sababu Mungu alimsaidia. Labani na wana wake walimuonea Yakobo wivu. Waliudhika kwa kuona ana kondoo na mbuzi wengi.

Mungu alizungumza na Yakobo kwa ndoto akisema, "Rudi kwa nchi ya Kanaani, nitakulinda."

Labani na wana wake walipokuwa wameenda kukata kondoo wao manyoya, Yakobo na familia yake waliondoka kwenda kwa nchi ya Kanaani.

Walipokaribia nchi ya Kanaani Yakobo aliogopa nduguye Esau. Esau bado amemkasirikia? Na bado anataka kumua? Esau atamuonea wivu kwa sababu Yakobo alikuwa tajiri wa n'gombe? Kuna malaika walioenda kukutana na Yakobo na kumwambia kwamba Mungu ako anamlinda.

Yakobo akatuma mjumbe aende amwambie Esau kwamba Mungu alikuwa amembariki. Akauliza Esau awe na amani naye. Mjumbe akarudi kwa Yakobo. Akumwambia kwamba Esau alikuwa anakuja na jeshi la wanaume 400 kukutana naye. Yakobo aliogopa.

Yakobo aliomba Mungu. Aliuliza Mungu amuokoe kutoka kwa Esau. Aligawanyisha mifugo yake na familia kwa vikundi viwili. Esau akikuja na aue kundi moja, kundi lingine litaokoka. Yakobo alipelekea Esau zawadi nyingi ili ampunguze hasira. Yakobo alimpelekea mbuzi 220 na watumishi. Wakamwambia Esau, "Hii ni zawadi ya bwana wangu Esau kutoka kwa mtumishi wako Yakobo." Tena akampelekea kondoo 220 na ujumbe huo huo. Tena akampelekea ngamia 30 na watoto wao, n'gombe 50 na punda 30. Kila kundi lilikutana na Esau na kumwambia, "Hii ni zawadi ya bwana wangu kutoka kwa mtumishi wako Yakobo."

Usiku huo Yakobo na wakeze walipiga kambi kando ya kivuko cha Yaboki. Malaika alimkujia Yakobo. Yakobo akamwomba malaika ambariki. Yakobo alijua kwamba alitakiwa usaidizi na baraka za Mungu sana kwa sababu asubuhi atakutana na Esau.
Yakobo aliendelea kumsihi malaika ambariki. Hangemuajilia malaika aende. Walishindana mpaka kukapambazuka. Kulipopambazuka malaika alimgusa paja la Yakobo na paja likateguka kwa kiungo.

Malaika alimuuliza, "Jina lako ni nani?" Yakobo alijibu, "Jina langu ni Yakobo." Malaika akamwambia, "Jina lako halitakuwa Yakobo tena. Mungu amebadilisha jina lako na utaitwa **Israeli** kwa sababu umeshindana na Mungu tena na mtu." Yakobo maana yake ni 'mdanganyi' – Yakobo alidanganya Isaka. Israeli maana yake ni 'Ukuu na Mungu.' Baadaye malaika akambariki Yakobo.

Yakobo alielewa kwamba hakuokoka kwa ajili ya nguvu yake mwenyewe. Ilikuwa uwezo wa Mungu uliomuokoa. Paja la Yakobo lilikuwa limeteguka kwa kiungo na alichechema akienda kukutana na Esau. Hangeweza kujitetea kwa nguvu zake. Lakini hakuogopa. Aliamini kwamba Mungu atamlinda. Yakobo alichechema kwa maisha yake yote. Ilimkumbusha kuwa na imani kwa Mungu.

Yakobo aligawanya familia yake kwa vikundi. Halafu akaenda kukutana na Esau. Esau hakukuwa na chuki tena. Alifurahi kumuona Yakobo na akamkumbatia. Esau alishangaa kuwaona wake na watoto wa Yakobo. Alifurahia zawadi zenye Yakobo alimtumanishia. Nyuma ya miaka ishirini Yakobo ailtoka Kanaani bila chochote. Sasa amerudi na n'gombe na kundi kubwa la mifugo. Alikuwa mtu tajiri.

Esau na Yakobo walikuwa marafiki tena. Esau alirudi nyumbani kwake kwa nchi ya Edomu. Yakobo alibaki kwa nchi ya Kanaani. Yakobo alimshukuru Mungu kwa kumrejesha kwa amani katika nchi ya *Kanaani*. Alishukuru Mungu kwa kumuezesha arudi kuishi kwa nchi aliyoahidi Ibrahamu na uzao wake.



YAKOBO AKUTANA NA ESAU

Yakobo alisafiri kutoka Harani kwenda kuishi nchi ya Kanaani

Esau alitoka Edomu na watu 400

Yakobo alishindana na Malaika kwa Kivuko cha Yaboki

Yakobo na Esau walikutana Kwa Kivuko cha Yaboki

Walikuwa marafiki tena